CHAPISHO LA KWELI

MUONGOZO WA REDIO

MAANDALIZI YA JAMII (KATIKA ENEO)

TANZANIA

UTANGULIZI

Maandalizi ya Jamii ni mchakato wa watu kuungana pamoja kufanya kazi kufikia lengo fulani au kufanya mabadiliko yenye athari nzuri. Kuandaa jamii kunaweza kuleta watu pamoja kuboresha nafasi yao, pamoja na ardhi na pia kushirikiana na jamii zingine ili kuandaa mabadiliko na kufanya kazi kwa ushirikiano mwema.

Vijana wana nguvu zaidi ya kuleta mabadiliko na pia kuandaa jamii zao. Hii inaweza kufanywa kwa njia kadhaa, ikiwa ni pamoja na kuunda harakati zinazoongozwa na vijana na kufanya kazi na mashirika au taasisi zisizo za kiserikali ambazo ziko kipaumbele kwa kupaza sauti za vijana katika jamii zao. Katika harakati zinazoongozwa na vijana, vijana wanaweza kufanya kazi pamoja ili kugawana majukumu tofauti ndio waweze kufikia malengo yao ya kuleta mabadiliko ya aina fulani. Kwa mfano, ikiwa kikundi cha vijana kilitaka kuchukua jukumu la kuhamasisha jamii yao ili kuchukulia suala la uchakataji kwa umakini zaidi, kuna majukumu na jitihada kadhaa za kuchukuliwa, ikiwa ni pamoja na chochote kutoka maandalizi ya kampeni katika mitandao ya kijamii, kuzungumza na manispaa, kuzungumza na majirani na pia kuwaongelesha wanajamii wenyewe.

Kuandaa jamii pia kunaweza kuwa kama kushirikiana au kupata msaada kutoka kwa mashirika yaliyopo au taasisi zisizo za kiserikali ili kusaidia kuchangia misaada ambayo umpendezwa kuiwajibikia. Katika mfano wa miradi wa Kuchakata taka, waandaaji wa jamii ya vijana wanaweza kufikia taasisi za haki za mazingira na kuomba nyenzo zinazohitajika kuanzisha uchakataji kama mapipa, au kutoa mafunzo katika kituo cha jamii kuhusu njia tofauti ambazo watu wanaweza kuchakata na kusindika vitu tofauti vya nyumbani.

Cha msingi katika maandalizi ya jamii ni ushirikiano, kwa sababu kila mtu anaweza kuchukua jukumu ambalo linamfaa zaidi na ambayo talanta zake zitachangia zaidi ili kuleta mabadiliko.

TAFSIRI

Uzalishaji huwa utoaji au uachiliaji wa vitu kama vile joto, kimiminika, gesi. Katika muktadha wa haki ya mazingira, uchafuzi mara nyingi huzungumziwa kwa kuitaja kama uzalishaji wa gesi ya kaboni au gesi nyingine chafu.

Mifumo ya Nishati Zinazoweza Kuzalishwa Upya (kusindikwa) ni vitu kama jenereta za upepo (wind generators), paneli zinazonyonya mwanga wa jua (solar panels), au mipango ya usafi wa mazingira ambayo husafishia watu maji ya mvua kwa matumizi salama. Mifumo hii yote hutumia rasilimali ambazo zinatoka kwenye vyanzo vya asili au michakato ambayo hujazwa tena kila wakati, kama mvua, upepo, na mwanga wa jua. Aina ya vyanzo hivi vya nishati hutoa faida za kiuchumi hasa kutoa nafasi za ajira, fursa za mafunzo na pia faida kubwa kwa mazingira.

KUTAMBUA MASUALA TATA: MABADILIKO YA TABIA NCHI YANAATHIRIJE JAMII YANGU?

Taka
Je, taka inasimamiwaje katika jamii yangu? Inasimamiwa vibaya kivipi? Maeneo ya utupaji taka au vifaa vya kutilia takataka katika jamii yangu viko wapi? Hatua za usafi katika jamii yangu ni zipi? Ni nini kinachokosekana au kinachoweka watu hatarini - iwe ni mifereji, maji safi, maji ya bomba, na vitu vingine vya aina hii?

Uzalishaji
Katika jamii yangu, ni nini husababisha uzalishaji usiofaa? Ni mashirika yapi au watu gani ambao nina weza kuzungumza nao kuhusu usimamizi wa uzalishaji usiofaa? Ni aina gani ya magari yaliopo katika jamii yangu? Ni majengo gani yanayofanya uzalishaji katika jamii yangu?

Usafiri
Watu katika jamii yangu hutumia usafiri wa aina gani? Watu katika jamii yangu hutumia usafiri wa pamoja kwa kiasi gani? Usafiri unachangiaje (au la) kwa suala la ongezeko la kiwango cha joto duniani?

Viwanda
Je, ni viwanda vipi ambavyo viko katika jamii yangu vinavyoathiri vibaya mazingira, kama vile ufugaji wa wanyama wengi, uchimbaji madini, viwanda vinavyozalisha taka au uzalishaji wa gesi chafu ya kaboni? Ni viwanda vipi vinavyozalisha vyanzo vya nishati ndani ya, au karibu na, jamii yangu?

Afya
Afya ya jamii yangu inaathiriwa vipi na mabadiliko ya tabia nchi? Je, ni mambo yapi yanahatarisha afya yangu na ya wengine inapofikia suala la mabadiliko ya tabia nchi? Mabadiliko ya tabia nchi yanaathirije afya ya utamaduni wetu, lugha, na hisia za jamii yetu? Jamii yetu imewajibikaje ili kupambana na hatari za kiafya, kama vile moto, mafuriko, au mtetemeko ya ardhi?

Usalama wa Chakula na Maji
Vyanzo vya chakula safi katika jamii yangu viko wapi? Maeneo ya uuzaji wa chakula kama vile masoko, maduka ya vyakula au vibanda yanaweza kusaidia jamii yangu kwa njia ambayo inahitaji? Kuna vyanzo vya chakula vya kutosha, pamoja na chakula bora (fresh) katika jamii yangu? Chakula cha jamii yangu kinachangiaje (au la) kwa mabadiliko ya tabia nchi? Chanzo cha chakula cha jamii yangu kitaathiriwa na mabadiliko ya tabia nchi?

Uchumi
Kuna aina gani za kazi na ajira katika jamii yangu? Kuna kazi za kudumisha/kuimarisha mazingira (green-jobs) katika jamii yangu - kazi ambazo zinachangia vyema kuleta mazingira na jamii endelevu? Kazi katika jamii yangu zitaathiriwaje na mabadiliko ya tabia nchi?

JE, NI SUALA GANI KUBWA AMBALO TUNAWEZA KUATHIRI ZAIDI?'

Mfano (Uchunguzi kifani): Uchakataji katika mji wa Cape Town
Yola Mgogwana, aliyezaliwa na kukulia mtaani wa Khayelitsha, mjini Cape Town, anatoa changamoto kwa jamii yake kutunza mazingira vizuri, na kuacha utupaji kiholela wa takataka, na pia matumizi ya plastiki zinazotumika mara moja tu. Yola, kama mwanafunzi wa darasa la tano, alichagua shule na jamii yake ili kuhamasisha jamii yake, familia na wenzake kuchakata, na pia kupunguza kiwango cha takataka katika eneo lao. Kila siku akienda shuleni, Yola hubeba mkoba mweusi kuokota takataka na chupa mitaani, na mnamo 2019, Yola, wanafunzi wenzake na karibu vijana wengine 2,000 waliandamana kwenda kwenye bunge la Cape Town kudai haki ya mabadiliko ya tabia nchi iwe kipaumbele nchini Afrika Kusini. Yola alitoa hotuba siku hiyo akimsihi rais, Cyril Ramaphosa, kuchukulia suala la mabadiliko ya tabia nchi kwa uzito ili kuhakikishia vijana maisha ya baadaye

Kuvumbua kile kinachopaswa kubadilika? (kipengele cha muundo)
- Utafiti mwafaka/kina
- Kutambua sababu zinazoathiri shida hizo
- Kutaja wadau husika

Nani atahusika na mabadiliko (hadhira wa kufikia) (kipengele cha muundo)
- Wasikilizaji wa vipindi vya redio
- Hadhira na washiriki wa shughuli za kijamii
- Washiriki katika mitandao ya kijamii

Nani atatusaidia kuleta mabadiliko (kipengee cha muundo)
- Badilisha ujumbe na ujumuishe taarifa za kweli na muhimu kuhusu masuala na jinsi ambavyo watu wanaweza kuhusika
- Kutambua washirika na wahusika
- Unda mipango ya hatua kusaidia maandalizi ya jinsi mchakato wa mradi (au miradi) itakavyokuwa

ATHARI: MIRADI YA VIJANA INAYOONGOZWA KATIKA BARA

Mfano (Uchunguzi kifani): Upandaji tena wa miti nchini Kenya
Elizabeth Wanjiru Wathuti alianzisha mradi wa “Green Generation Initiative” nchini Kenya mnamo 2016, kama njia ya kuhamasisha vijana wengine wanaotaka kuchukua hatua za kuwajibikia mabadiliko ya tabia nchi na afya ya mazingira. Elizabeth alikuwa na miaka 7 wakati alipanda mti wake wa kwanza, na katika shule yake ya upili alianzisha kikundi cha kulinda mazingira. Baada ya shule ya upili, akiwa na miaka ishirini, ndio wakati alipoanzisha “Green Generation Initiative” kama sehemu ya dhamira ya shirika lake, ambayo ni kurejesha “kijani” katika shule nchini kwake kwa kupanda miti. Wanjiru alizaliwa na kukua katika eneo la Nyeri, ambayo ina umaarufu wa kuwa na msitu zaidi nchini Kenya. Hadi sasa, mradi huo wake umepanda zaidi ya miti 30,000.
- **https://www.instagram.com/ggi_kenya/**

FAIDA KUTOKA KWA MABADILIKO YALIYOONGOZWA NA VIJANA:

Mtazamo mpya

Inapofikia suala la mabadiliko kwa kijamii, vijana mara nyingi wanaweza kuleta mtazamo mpya. Vijana wanaweza wakawa na uzoefu mdogo wa kuwa katika sehemu za mifumo fulani au utekelezaji wa majukumu fulani, lakini hata hivyo vijana wengi wanaweza pia kutaja na kutambua masuala yaliyo karibu nao. Kwa mfano, wanafunzi watoto wanaweza kustahili kutambua mifumo bora ya uchukuzi wa shule kama watu ambao wanapaswa kuitumia kila siku, iwe ni kushinikiza mabasi au dala-dala zinazozalisha uchafu kidogo, au njia zinazojumuisha zaidi. Vijana wana uharaka zaidi pia, ikilinganishwa na watu wazima, na wanaweza kushinikiza mabadiliko yatekelezwe mapema.

Mahusiano kidogo na miundo iliyopo

Wakati vijana wengi wanaweza kuchukua majukumu makubwa katika familia au jamii zao kama vile kuwa wahudumu au kufanya kazi nyingi, vijana wengi hawana uhusiano na miundo iliyopo. Kwa mfano, kwa sababu vijana kwa ujumla wana uhusiano mdogo wa serikali na matumizi ya serikali juu ya fedha, wanaweza kushawishi mabadiliko kwa mifumo ya nishati mbadala bila upotezaji au kujitolea zaidi kwa udumishaji wa mfumo uliopo. Mara nyingi, serikali hazifanyi mabadiliko yanayosaidia mazingira katika mifumo ya nishati, kama mafuta asili (fossil fuels) kwa sababu viwanda hivyo huleta faida na pesa kwa wale wanaohusika.

Mara nyingi kuna msaada wa harakati na miradi ya (na inayoongozwa na) vijana

Mara nyingi, jamii inaweza kuangalia vijana kwa jinsi wanavyochangia kuleta mabadiliko. Kwa mfano, mnamo Septemba 2019, mamia ya wanafunzi mjini Delhi

nchini India, walikosa kwenda shule na kuandamana hadi kwa serikali ya mitaa na kutaka mabadiliko ya tabia nchi yaanze kuchukuliwa kwa uzito zaidi, kama sehemu ya harakati ya kimataifa ya #Ijumaa (#FridaysforFuture international movement). India ni nchi ambayo imekuwa ikikumbwa na athari mbaya za mabadiliko ya tabia nchi pamoja na mawimbi ya joto lenye nguvu na la kuua, dhoruba mbaya, upungufu wa maji na ukame. Kutokana na haya, vijana wamekuwa wakiandamana kwa idadi kubwa kudai serikali za mitaa na kitaifa kuchukua hatua. Aina hii ya maandamano na kudai hatua imesaidiwa na waelimishaji na walimu ambao huhimiza na kuwapa wanafunzi nafasi ya kukosa shule ili waandamane na kupaza sauti zao zisikike kote. Zaidi ya hayo, maandamano yao yamehudhuriwa na watu wazima na wanajamii wengine pia katika miji kadhaa.
- **https://www.timesnownews.com/mirror-now/in-focus/photo-gallery/photos-fridays-for-future-citizens-take-over-delhi-streets-as-they-join-the-global-climate-change-strike/496679**

CHANGAMOTO ZA MABADILIKO YALIYOONGOZWA NA VIJANA:

Watu wazima huwa hawasikilizi vijana kwa ajili ya umri wao

Wakati mwingine vijana hupuuzwa kwa sababu ya umri wao na kwa “kutokuwa na uzoefu mwingi” wakati wanapojaribu kubadilisha mambo ndani ya jamii zao. Vijana wanaweza kupata upinzani au ukosefu wa msaada kutoka kwa watu wazima kutokana na mitazamo kama hii.

Kutojua katika suala la maandalizi au shughuli za upangaji kwa sababu ya ukosefu wa uzoefu thabiti

Vijana mara nyingi wanatamani na kuwa na uelewa, lakini kama waandaaji wengine wowote, wanaweza kufanya makosa. Kwa sababu vijana wanaweza kuwa ndio tu wanaanza mradi wao wa kuandaa jamii, wanaweza kutofahamu yote yanayoweza kufanya mradi uendelee vizuri. Kwa mfano, wakati mwingine suala la usafirishaji (wa watu) halizingatiwi wakati wa kuandaa jamii, na kujua jinsi ya kusimamia hiyo itahakikisha kuwa wanajamii wanaweza kuhudhuria mradi wako. Kwa mfano ikiwa unaandaa sherehe ya siku ya kupanda miti, suala la usafirishaji ni la muhimu sana ili watu waweze kuhudhuria - lakini vidokezo kama hivi vyote huja kutokana na uzoefu.

Inaweza kuwatenga watu wazee na mifumo mingine ya msaada

Wakati mwingine vijana wanapoanza harakati za kuandaa jamii, wanaweza kusahau kujumuisha mitazamo na sauti fulani kwa sababu wanalenga maswala yaliyoongozwa na vijana au masuala ya vijana. Maandalizi ya jamii inayoongozwa na vijana ina nguvu sana, lakini ikiwa haijumuishi sauti zote katika jamii hiyo (kama sauti za watu wazima na pia wale ambao wanahisi tofauti), inaweza kutenga au kuregeleza mikazo katika masuala kadhaa.

Mfano (Uchunguzi kifani): Kampeni ya Kimataifa ya Mazingira inayoongozwa na Vijana
Mojawapo ya harakati inayojulikana sana ya haki za mazingira inayoongozwa na vijana inajulikana kama "Fridays for Future." Ilianzishwa Uropa, na sifa kwake mwanaharakati kijana Greta Thunberg ambaye alianza mgomo wa shule ili kuangazia mabadiliko ya tabia nchi. Kwa muda wa kipindi cha wiki tatu kabla ya uchaguzi wa Uswidi, alikuwa akikaa nje ya Bunge lao kila siku ya shule, akitaka hatua zichukuliwe kuhusu mabadiliko ya tabia nchi. Kutokana na mgomo wake, mtandao na harakati za kimataifa zilianza na vijana waandalizi kote ulimwenguni pia wakaanza migomo yao ya shule na mabadiliko ya tabia nchi. Mgomo wa kimataifa wa mabadiliko ya tabia nchi uliandaliwa na wanafunzi tarehe 29 Novemba 2019, ambapo migomo 2,200 iliandaliwa katika nchi 125, na zaidi ya vijana wagomaji milioni moja wakishiriki kutoka maeneo tofauti kama Ulaya, India, na nchi mbalimbali za bara la Afrika. Hii ilitendeka sanjari na mkutano "COP25" mjini Madrid, ambao ulikuwa mkutano mkubwa wa mabadiliko ya tabia nchi kati ya viongozi wa ulimwengu wa Umoja wa Mataifa. Vijana walijitokeza kwenye hafla na kudai mabadiliko ya tabia nchi yazingatiwe kwa uzito, kwamba vyanzo vya nishati mbadala vichukuliwe ulimwenguni, pamoja na kuaagiza yafuatayo:

- Kudumisha kiwango cha joto ulimwenguni kuwa chini ya 1.5 °C.
- Kuwe na haki za mabadiliko ya tabia nchi na usawa kwa kila mtu.
- Mkataba wa Paris ufuatwe.
- Kuunga juhudi za kisayansi.

HARAKATI ZA VIJANA

Je, tunawezaje kubadilisha mambo? (Jinsi tunavyoweza kujiandaa)

- **Kuzungumza kuhusu mabadiliko/matumizi ya redio (kushiriki ukweli muhimu)**
- **Kuripoti kuhusu mabadiliko yanayotokea**
- **Kuchukua hatua**
- **Kutumia mitandao ya kijamii**
- **Kuandaa hafla - huku tukiendelea kuzingatia mikakati ya utengaji wa nafasi ya kijamii ipasavyo (social distancing)**
- **Kutokea kwa umati wa ghafla (flash mob)**
- **Kuandamana**

Mfano:
Vijana waliongoza Usafishaji na Usafi wa Mazingira nchini Nigeria
"U-Recycle Initiative Nigeria" ni kikundi cha zaidi ya vijana 40 ambao wana shauku ya kukuza uchakataji endelevu nchini Nigeria. Kikundi hiki kilianzishwa na Moejoh Oluwaseyi, mwanaharakati wa vijana aliye na miaka 17. Wakati alikuwa akishirikiana na taasisi isiyo ya kiserikali iitwayo "The Nigerian Child Initiative," na shule yake, Oluwaseyi aliweza kuanzisha kilabu/kikundi cha mazingira ili kuanza kuandaa juhudi za usafishaji wa ufuo wa bahari, miradi ya kuchakata, na warsha ambazo zinaunganisha usimamizi wa taka na maji safi, na jinsi vijana wanaweza kuandaa maisha bora ya baadaye. Oluwaseyi na kikundi chake wanahusika katika kuandaa

warsha, kusaidia vilabu/vikundi vya mazingira, ujenzi wa “U-Recycle Hubs” ambazo ni za kutenganisha taka, kuandaa mashindano, matembezi ya uhamasishaji, usafishaji wa ufuo wa bahari na mengi zaidi.

Kulenga wapi: (kipengee cha muundo)

- Nyumbani
- Shuleni
- Barabarani
- Kwenye mitandao ya kijamii
- Katika nafasi ya umma
- Katika nafasi ya kibinafsi

Tutajuaje wakati imebadilika? (kipengee cha muundo)

- Watu zaidi watafahamu suala hilo
- Watu watatenda tofauti/kubadilisha mienendo yao
- Je, ni nini kitakacho kuwa tofauti?

ONDOA HADITHI POTOFU (UZUSHI), PATA UKWELI

UZUSHI	UKWELI
Vijana hawawezi kubadilisha mambo, hawana sauti wala nguvu	Vijana wanaweza kuleta mabadiliko kabisa, na wanaweza kuanza toka mahali popote. Kwa mfano, mnamo mwaka wa 2016, kikundi cha vijana cha Wamarekani asili (native Americans) nchini Amerika kilisaidia kuzindua na kuunga mkono sana maandamano makubwa dhidi ya utekelezaji wa bomba ambalo lingebeba mafuta chini ya ardhi, ikitishia sana ardhi asili na takatifu ya makabila mengi katika eneo la Dakota Kusini, ambayo ni kabila la "Standing Rock Sioux." Kikundi cha vijana cha "One Mind Youth Movement" kilikita kambi na duru za maombi humo "Standing Rock." Mwisho wa 2016, kambi za Rock Rock ziliongezeka hadi zaidi ya 10,000, zilizojazwa na watu wa asili kutoka mamia ya mataifa, wanaharakati wa mabadiliko ya tabia nchi, na vikundi vingine na pia watu ambao walikuwa tayari kutetea ardhi na afya ya dunia. Vijana katika kesi hii walichochea harakati ambazo zilipata umakini wa kitaifa, na vile vile msaada wa kimataifa, na mnamo 2021, rais mpya wa Amerika akageuza kibali ili bomba hilo lisiendelee kujengwa. (New York Times)
Huchukua muda mrefu ili mabadiliko itokee	Mabadiliko mengine hufanyika kwa muda na mengine kwa haraka sana. Kama tu vile mtazamo wako kuhusu kitu unaweza kubadilika kwa dakika moja, huo pia ni mwanzo wa mabadiliko. Kwa mfano, ili kupambana na janga la COVID-19, Vittorio Foglio na kikundi chake cha wanaskauti cha wavulana (boy-scouts) mjini Geneva nchini Uswizi, walijipanga na kushirikisha watu wengine kupelekea watu wazee katika jamii yao vifaa na vyakula. Huku kuhamasisha watu wengine na wakala pia kushiriki na kuleta mabadiliko katika jamii, kwenyewe ni hali ya mabadiliko pia. (UN)
Kama mtu binafsi sina uwezo wowote wa kubadilisha chochote	Watu binafsi wanaweza kuleta mabadiliko, kama vile kuanzisha mradi au kusafisha mtaa wako, lakini mabadiliko huwa makubwa zaidi wakati watu wengine wanajiunga na kufanya kazi pamoja. Kitu rahisi sana kama kuokota takataka katika eneo lako na kushirikisha watu wengine kukusaidia kinaweza kuwa na athari nzuri na kubwa. Kwa mfano, mnamo 2008 nchini Estonia, watu 50,000 walikuja pamoja kufanya mradi mkubwa wa kusafisha , ambapo watu katika jamii zao kote nchini waliungana na kutekeleza zoezi kubwa la usafishaji taka kwa siku nzima. Hii ilisababisha harakati ya Siku ya Usafi Duniani (World CleanUp Day) ambapo nchi nyingi hutekeleza siku za usafishaji. (Letsdoitworld)

Vijana hawawezi kuleta mabadiliko makubwa

Vijana wanaweza kujiandaa katika jamii zao kwa haki za mazingira, na wakati mwingine kazi kama hiyo inaweza kuathiri jamii jirani au kuvuma na kusikika ulimwenguni kote. Kwa mfano, Oladosu Adenike, mwanaharakati kijana wa mabadikilo ya tabia nchi kutoka Nigeria, alianza kuona madhara ya mabadiliko ya tabia nchi katika jamii yake wakati mafuriko ya mara kwa mara yalipoanza kutokea. Yeye huandaa mabaraza ya kuelimisha jamii, ambapo hutembelea shule na maeneo mengine ya umma ili kuelimisha watu kuhusu mabadiliko yatabia nchi. Pia anaelimisha wanajamii kuhusu uhusiano uliopo kati ya hatua za mabadiliko ya tabia nchi, umaskini na haki za wanawake. Kwa sababu ya kazi yake, alikua balozi wa harakati tofauti kama “Fridays for Future,” “Earth Uprising,” na “African Youth Climate,” na ameweza kuipaza sauti yake kupitia majukwaa haya ya kimataifa na vile vile kupitia kwa wanahabari na mashirika mengine, kama “GreenPeace.”

Pata taarifa zaidi kuhusu Oladosu hapa:
https://www.queenscommonwealthtrust.org/inspiration/oladosu-adenike-i-lead-climate-nigeria-lake-chad/

JE, WAJUA? (TANZANIA)

Tanzania ni nchi ya watu milioni 55, na milioni 28 wako chini ya miaka 25. Na zaidi ya nusu ya idadi ya watu wakiwa ni vijana, Tanzania ni moja ya nchi duniani zenye idadi kubwa zaidi ya watu wenye umri mdogo.

Kati ya miaka ya 2017 na 2020, katika vijiji 4 vya Tanzania, vijana wanaojitolea kwa kushirikiana na taasisi zisizo za kiserikali walitengeneza vitalu vya miti ambapo miche zaidi ya 300,000 ilipandwa.

Mnamo mwaka wa 2019, kikundi cha vijana kilikusanyika pamoja kuandaa mradi uitwao Kambi ya Vijana ya Afya ya Uzazi na Haki (Sexual Reproductive Health and Rights Youth Camp). Kambi hii inajumuisha watu katika mikoa 14 tofauti nchini kote kwa zana za kushiriki uzoefu wao katika masuala ya afya ya uzazi, kama vile GBV (dhuluma za kijinsia), ukeketaji, VVU na upangaji wa uzazi.



Umoja wa Vijana Tanzania (Tanzania Youth Coalition) ni kikundi cha utetezi kinachoongozwa na vijana kilichoanzishwa mnamo 2002 na vijana kumi. Hadi leo, mifumo ya muungano na washirika wa nchini na wa kimataifa hutekeleza miradi katika nyanja tofauti kama vile kilimo, upishi, na sera.

Mfano (Uchunguzi kifani):
Mnamo 2019, kikundi cha vijana katika kijiji cha Ofua 2 nchini Uganda kilianza kukusanya taka za plastiki kila Jumamosi ili kutengeneza vifaa vya ujenzi. Kikundi cha vijana kiligundua kuwa mifuko ya ufungaji bidhaa au chakula, viti vilivyovunjika, vyombo na chupa za soda na maji, ndio wingi wa taka ambayo iko katika jamii yao, kwa hivyo walishirikiana na taasisi isiyo ya kiserikali la eneo hilo ili kuokota taka hizo na kuiyeyusha kuwa matofali. Hii ilileta mabadiliko makubwa katika jamii yao kwa kupunguza taka inayoonekana na pia kwa kulinda wanyama wasimeze plastiki.

(Source; Youth for Nature)

RASILIMALI

- **Mazingira ni Kitovu cha Maendeleo Tanzania**
- **Fridays for Future**
- **Global Citizen**
- **Youth Led Community organising Strategies and Tools**
- **Global Change Makers Toolkits**

COMMUNITY ORGANISING (LOCAL LEVEL)

MUONGOZO WA REDIO

MADA MAHUSUSI

“NJIA TOFAUTI ZA KUZUNGUMZA KUHUSU MAANDALIZI YA JAMII”

- Kuandaa jamii ni nini? Kwa nini ni muhimu kuzungumza kuihusu na uhusiano wa vijana?
- Kuna mifano ipi ya maandalizi ya kijamii katika jamii yako?
- Ni kwa watu wazima tu ambao hujiandaa, au vijana pia hujiandaa vilivyo?
- Kuna miradi ya kijamii ya vijana katika shule yako, au katika jamii yako?
- Ni mambo yapi ambayo huwazuia vijana kufikiria kwamba wanaweza kuleta mabadiliko katika jamii zao?
- Vijana wanawezaje kufanya kazi pamoja na watu wazima wakati wa maandalizi ya kijamii? Je, utatunzaje juhudi za maandalizi ya jamii ili iwe inaweza kufikia na kushirikisha watu wa kila kizazi na wenye uwezo mbalimbali?

CHAGUA MADA MAHUSUSI (KUTOKA ORODHA ILIYOPO)

(Taja jina la mada mahusui ambayo umechangua) kwa mfano. “Kuandaa jamii ni nini? Kwa nini ni muhimu kuzungumza kuihusu na uhusiano wa vijana?”

NJIA TOFAUTI ZA KUZUNGUMZA KUHUSU (TAJA MADA MAHUSUSI ULIYOCHAGUA) KWA MFANO. “Kuandaa jamii ni nini?”

- Kuna maandalizi yapi tofauti ya kijamii? Ni mifano gani ya kuandaa jamii unaweza kuifikiria?
- Ni athari zipi nzuri ambazo wameweza kuleta kupitia juhudi zao za maandalizi ya jamii ?

MIUNDO YA VIPENGELE VYA KIPINDI CHA REDIO

SAUTI ZA UMMA

Lengo la sauti za umma
Kupata maoni mengi kuhusu mada moja

Utazungumza na nani?
Mtu yeyote kutoka kwa jamii, kwa mfano shuleni.

Swali
Ni miradi ipi inayoongozwa na vijana katika jamii yako?

MAONI YA SAUTI

Lengo la maoni ya sauti:
Kupata maoni ya watu kuhusu mada ambayo wanaijali.

Utazungumza na nani?

- Mwakilishi wa taasisi lisilo la kiserikali ambaye kazi yake inajumuisha kusaidia vijana na/au haki ya mazingira;
- Mwanaharakati kijana katika jamii yako; na
- Mwanajamii ambaye ni mratibu wa maandalizi, haswa katika haki ya mazingira au tabia nchi.

Changio za mazungumzo:

- Kuandaa jamii ni nini ? Vijana wanawezaje kuwa waandaaji na kushiriki vyema katika jamii yao?
- Ni miradi ipi ya kuandaa jamii inayoongozwa na vijana ambayo imeweza kufanikiwa au inaendelea?
- Kwa nini ni muhimu kwa vijana kujisikia wanauwezo wa kuleta mabadiliko katika masuala ya haki ya mazingira na tabia nchi?
- Ni maoni yapi potofu ya kawaida yanayohusu jinsi mabadiliko yanavyotekelezwa?
- Ni makosa gani ya kawaida ambayo watu wanaweza kufanya wakati wanandaa jamii? Watu wanawezaje kuepuka makosa haya?
- Ni mifumo ipi endelevu ya mazingira ambayo vijana wanaweza kuilenga katika juhudi zao?
- Vijana wanawezaje kufanya kazi na watu wengine kwa maandalizi yao, ikiwa ni pamoja na watu tofauti wenye uwezo mbalimbali na watu wazima?
- Kuna faida gani za kufanya kazi pamoja ili kuleta mabadiliko yanayozuia mabadiliko ya tabia nchi?

TANGAZO LA UMMA

Lengo la Tangazo la Umma:
Kuweka mwamko wa jamii kuhusu jambo fulani.

Unda tangazo la umma (PSA) linaloamsha mwamko kuhusu umuhimu wa kuzungumza na vijana kuhusu (mada inayohusiana na ukataji miti/urejeshaji wamisitu).

Mfano:
Sauti 1: Khamisi, je, unafikiri kwamba vijana wanaweza kuleta mabadiliko muhimu katika jamii zetu, haswa tunapofikia suala la mabadiliko ya tabia nchi?
Sauti 2: Naam, lakini wakati mwingine nadhani sisi hufanywa kusikia kama ni tatizo kuwa
Sauti 1: Mimi pia, lakini vijana wana uwezo wa kujiandaa vyema katika jamii yetu ili kuleta mabadiliko madogo ambayo ni changio mwafaka kwa maendeleo makubwa
Sauti 2: Hiyo ni kweli, tunaweza kuleta mabadiliko!
Wito (kauli mbiu): Jiandaeni kwa mabadiliko mazuri, juhudi zote ni za thamani!

WASIFU WA SAUTI

Lengo la wasifu wa sauti:
Wasikilizaji wasikie hadithi ya kuhamasisha kuhusu mada ya kipindi.

Who do you talk to?

- A local farmer who can share their experience of trying to deal with issues regarding lack of access to water. Ask them how they make sure they have enough water for their farm, and what strategies they use to save water.
- A community member who can share their experience of how they collect, store and save water in their home.

Utazungumza na nani?

- Kijana mhusika katika maandalizi ya jamii, kama vile mradi wa shule;
- Mwalimu anayetetea vijana wanaoleta mabadiliko; na
- Mfanyakazi wa taasisi lisilo la kiserikali katika nyanja ya mazingira ambaye ana uzoefu wa kusaidia vijana kuandaa na kutekeleza miradi.

MAANDALIZI YA KIPINDI CHAKO

Tumia miundo ya vipengele vya kipindi cha redio, utafiti wako na maandalizi yaliopendekezwa ili kuunda kipindi chako.

[KUFUNGUA KIPINDI]
Mtangazaji 1: Imetimia [TAJA SAA]. Karibu ujiunge nasi kwenye makala ya [TAJA JINA LA KIPINDI] hapa [TAJA JINA LA STESHENI]. Mimi ni [TAJA JINA LAKO]

Mtangazaji 2: Na jina langu ni [TAJA JINA LAKO]. Kwenye makala ya leo, tutazungumzia kuandaa jamii.

Mtangazaji 1: Lo! Hiyo ni mada ngumu! Jameni, tutaanzia wapi?

Mtangazaji 2: Si tuanze kwa kutafsiri maana yake?

Mtangazaji 1: Naam, basi twende kazi !

Mtangazaji 2: Ngoja nianze kwa kuwapa mfano. Unakumbuka ile taasisi isiyo ya kiserikali ambayo nilikuwa ninakuelezea? Abalimi?

Mtangazaji 1: Ehe, ile ambayo inatoa mafunzo ya kilimo cha mijini?

Mtangazaji 2: Ndio! Inawafunza watu jinsi ya kupanda na kudumisha bustani za mboga katika jamii zenye shida huko mjini Cape Town. Wanasaidia bustani za watu za nyumbani, jamii na bustani ambazo pia zinalengo la kuleta mapato.

Mtangazaji 1: Aha, kwa hivyo mratibu wake amegundua shida ya uhaba wa chakula na ukosefu wa ajira katika jamii hii. Na zana za bustani na msaada wa mradi ndio jinsi wamejipanga ili waweze kushughulikia shida hiyo maalum?
And the gardening tools and support program is how they have organised to address that specific problem?

Mtangazaji 2: Naam, kabisa!

Mtangazaji 1: Kwa hivyo, kuandaa jamii, kama walivyofanya katika mfano huu, ni aina mojawapo ya harakati za kufanya mabadiliko chanya kwa pamoja?

Mtangazaji 2: Naam! Ndivyo hivyo! Kuandaa jamii, haswa vijana, kunaweza kuwa mambo kama kuanzisha mradi wa kuchakata taka shuleni kwao. Kilicho kizuri katika shughuli ya kandaa jamii ni kwamba kila mtu anaweza kuchukua jukumu lile ambalo linamfaa zaidi kwa masilahi yake, au uwezo wake. Tumia kile unachojua na kile ulicho nacho tayari, na kisha mkijenge na kukiboresha zaidi.

Mtangazaji 1: Naona! Kwa hivyo pia watu wengine wanaweza kufanya harakati katika mitandao ya kijamii, na wengine wanaweza kuwa na jukumu la kutafuta vifaa, huku wengine wakiwajibika kutafuta watu wengine wahusike, n.k.

Mtangazaji 2: Ndio! Kuandaa jamii hata kunaweza kukawa na athari nzuri ulimwenguni kote. Kinachohitajika ni vijana kutoa hadithi zao kwa wengine ili nao pia waone jinsi wanavyoweza kuiga na

MAANDALIZI YA KIPINDI CHAKO

Tumia miundo ya vipengele vya kipindi cha redio, utafiti wako na maandalizi yaliopendekezwa ili kuunda kipindi chako.

kufanya juhudi zao hivyo hivyo!

Mtangazaji 1: Hiyo ina maana sana, na inahamasisha zaidi kuona njia ambazo tunaweza kuletea jamii zetu athari nzuri. Vijana kweli wana uwezo wa kujitokeza, kujiandaa, na kufanya kazi pamoja,, na vile vile na watu wazee, ili kuleta mabadiliko.

Mtangazaji 1: Nadhani hii ni fursa nzuri ya kusikia kutoka kwa wasikilizaji wetu. Tungependa kusikia kutoka kwako. Je, umehusika vipi katika kuandaa jamii yako? Kuna suala la mazingira ambalo unadhani unaweza kulibadilisha ili kuleta mema?

[TAJA ANAYEHOJIWA]
[CHEZ MAHOJIANO]
[SHIRIKISHA WASHIRIKI WAKO KWA KUULIZA]

Mtangazaji 1: likuwa vizuri kusikia kutoka kwa wasikilizaji wetu. Ninapenda sana kusikia kuhusu jinsi wasikilizaji wetu wamehusika katika kuandaa jamii, na somo zao ambazo pia wamezishiriki.

Mtangazaji 2: Mimi pia, na kwa kweli inaonyesha kwamba tunaweza kuanza hivi leo kufanya mabadiliko katika jamii zetu na kulinda afya ya mazingira yetu.

Mtangazaji 1: Mazungumzo ya leo yamekuwa ya kuelimisha na kusisimua kabisa! Jiunge nasi wiki ijayo siku ya [TAJA SIKU na SAA ZA KIPINDI]. Tutazungumza kuhusu [TAJA MADA YA KIPINDI CHA WIKI IJAYO]. Hadi wakati huo, kwaheri!

MAANDALIZI YA KIPINDI CHA REDIO



MAADILI NA IDHINI

Hii inaweza kuwa mada nyeti kwa wengine, kwa hivyo hakikisha umewafahamisha wasikilizaji wako kuwaheshimu wale watakaotoa simulizi zao za kibinafsi.